

## MATUMIZI BORA YA MBOLEA YA MINJINGU KWENYE KILIMO CHA MBOGA



**Kimetayarishwa na :**

**Kituo cha Utafiti wa Mazao Mikocheni**

Simu: +255 22 2700552

Barua pepe: [mari@mari.org.tz](mailto:mari@mari.org.tz)

Nukushi: +255 22 2775549

**Kituo cha Utafiti wa Mazao Uyole**

Simu: +255 25 2510062

Nukushi: +255 25 2510065

Barua pepe: [ariuyole@iwayafrica.com](mailto:ariuyole@iwayafrica.com)



### Utangulizi

Minjingu ni mbolea asilia ya kupandia. Mbolea hii inatokana na miamba inayochimbwa katika eneo la Minjingu mkoani Manyara ambayo husagwa na kufungashwa kwenye kiwanda kilichojengwa katika eneo hilo. Mbolea ya Minjingu ina kirutubisho cha mimea aina ya fosiforasi kati ya asilimia 12.3-13.2. Tofauti na mbolea nyingine za kupandia zenye madini ya fosiforasi kama vile TSP na DAP ambazo huagizwa nje ya nchi hivyo kugarimu fedha nyingi za kigeni, mbolea hii inayopatikana hapa nchini bei yake ni nafuu.

### Udongo unaofaa kwa matumizi ya mbolea ya Minjingu

Mbolea ya Minjingu hufanya kazi vizuri katika udongo wenye kiwango kikubwa cha uchachu (pH) kuanzia 5.5 na kushuka chini na wenye kiasi kidogo cha madini ya kalsiamu. Uchachu wa udongo unaweza kujulikana kwa kupima sampuli kwenye maabara ya udongo. Tafiti zimeonesha kuwa uchachu wa udongo unasaidia kuyeyusha madini ya fosiforasi yaliyopo kwenye mbolea ya

Minjingu hivyo kuyafanya yapatikane na kunyonywa kwa urahisi na mizizi ya mimea. Pia mbolea hii huyeyuka vizuri katika udongo wenye unyevunyevu wa kutosha.

### Faida inayotokana na matumizi ya mbolea ya Minjingu

Mbolea hii huongeza mavuno ya mazao kwa kiwango kikubwa. Licha ya kirutubisho cha fosiforasi kinacholengwa kwenye mbolea hii, vipo pia virutubisho vingine muhimu kwa ustawi wa mimea. Kirutubisho cha fosiforasi huimarisha mizizi wakati mimea inapokua, hivyo kuiwezesha mimea kunyonya maji pamoja na virutubisho kwa wingi toka ardhini na kustahimili zaidi hali ya ukame.

Mbolea hii huyeyuka taratibu hivyo kudumu muda mrefu katika udongo baada ya kuwekwa. Huwa haizamishwi kirahisi na maji kwenda kwenye matabaka ya chini ya udongo hivyo husalia kwa muda mrefu hadi pale mmea utakapoitumia.

Mbolea ya Minjingu ni rahisi kuihifadhi na haina madhara kwa udongo kama mbolea nyingi za chumvi chumvi.

## **Kanuni za matumizi ya mbolea ya Minjingu katika kilimo cha mazao aina ya mboga**



Mimea aina ya mboga huhitaji kiwango cha kutosha cha madini ya fosiforasi. Ili kupata matokeo mazuri unapotumia mbolea hii, ni muhimu kuzingatia kanuni zote za kilimo bora mfano kuandaa shamba vizuri, kutumia mbegu bora, palizi kwa wakati, kuzuia wadudu waharibifu, magonjwa n.k. Ili mboga zipate kustawi vizuri chagua mbegu bora na zisizo na magonjwa, andaa bustani au shamba vizuri kwa kulima na kuondoa magugu yote. Kisha andaa matuta vizuri kwa kutifua na kusawazisha na kupiga haro. Kiasi cha mbolea ya Minjingu cha kuweka kwenye mboga hutegemea aina ya mboga inayopandwa. Kiasi cha kilo 100 kwa hekta (kilo 40 kwa ekari) kinatosha kwa mboga aina ya nyanya, mchicha na kabichi.

## **Matumizi wakati wa kupanda mboga**

Piga mashimo kwa nafasi zilizoshauriwa na kisha weka mbolea ya Minjingu katika kila shimo kwa kiwango kilichoshauriwa. Fukia kidogo ili isigusane na mizizi ya

miche ya mimea michanga kisha panda mimea na kufukia mizizi vizuri. Kama ni katika sesa, mwaga mbolea kiwango kilichoshauriwa kisha isambaze ili ichanganyike vizuri na udongo. Hii ifanyike hasa kwa mboga kama mchicha, halafu mwaga mbegu kwa kutawanya kwa kiwango kinachopendekezwa. Kama mbolea ya samadi iliyooza vizuri au mboji inapatikana inaweza kuchanganywa na mbolea ya Minjingu kwa matokeo mazuri zaidi. Samadi au mboji itatoa uchachu ambao utasaidia kuyeyusha mbolea ya Minjingu na kufanya virutubisho vilivyomo katika mbolea hiyo kupatikana kwa haraka zaidi.

Matokeo ya utafiti yameonyesha kuwa mboga zilizopandwa kwa kutumia mbolea ya Minjingu iliyochanganywa na mboji zilizaa zaidi kuliko zile zilizowekewa Minjingu peke yake .



## **Udhibiti wa wadudu waharibifu na magonjwa**

Kagua bustani mara kwa mara ili kugundua kama kuna wadudu waharibifu au magonjwa yanayoshambulia mboga zako. Dhibiti wadudu waharibifu kwa kutumia kiwango sahihi cha mwarobaini au viuatilifu salama vinavyopatikana madukani.

## **Kwa mawasiliano:**

Simu: +255 25 2510062

Nukushi: +255 25 2510065

Barua pepe: [ariuyole@iwayafrica.com](mailto:ariuyole@iwayafrica.com)

Simu: +255 22 2700552

Barua pepe: [mari@mari.org.tz](mailto:mari@mari.org.tz)

Nukushi: +255 22 2775549

